

MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2024

Kwa mujibu wa Kanuni ya 9 (1) ya Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji katika Mamlaka za Wilaya Tangazo la Serikali Namba 571 tarehe 12.07.2024, Msimamizi wa Uchaguzi amepewa mamlaka ya kutoa maelekezo kuhusu uchaguzi. Maelekezo haya yanatolewa siku sitini na mbili kabla ya siku ya uchaguzi, kwa lengo la kuhakikisha kuwa taratibu zote zinafuatwa na kwamba wapiga kura pamoja na wagombea wanapata taarifa zote zinazohitajika kwa wakati.

Maelekezo haya yanafafanua hatua zitakazoongoza mchakato wa uchaguzi, kuanzia uandikishaji wa wapiga kura, uchukuaji na urejeshaji wa fomu za kugombea, uteuzi wa wagombea na tarehe ya siku ya uchaguzi. Maelekezo haya yanalenga kutoa mwongozo ili kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa uwazi, haki na usawa na kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa.

(a) Tarehe ya Uchaguzi:

Kwa mujibu wa Tangazo la uchaguzi lililotolewa kwa kuzingatia kanuni ya 4 ya Kanuni za uchaguzi wa viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Tangazo la Serikali Na. 571, uchaguzi utafanyika tarehe 27 Novemba 2024.

(b) Muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura:

Kwa mujibu wa Kanuni ya 11 (GN. Na. 571/Mamlaka za Wilaya na GN Na. 574 (Mamlaka za Miji Midogo), zoezi la uandikishaji wa wapiga kura litafanyika kuanzia tarehe 11 hadi 20 Oktoba 2024 katika vituo vilivyopangwa.

(c) Muda na mahali pa kufanya uchaguzi:

Kwa mujibu wa kanuni ya 31 GN Na. 571 na 574 na Kanuni ya Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Kijiji, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa halmashauri ya Kijiji utafanyika kwenye vitongoji na vituo vingine vilivoelekezwa katika vijiji husika. .

(d) Wito kwa Wakazi wenyе sifa za kupiga kura:

Kwa mujibu wa kanuni ya 13 GN. Na. 571 na 574 wakazi wote wenyе umri wa miaka 18 au zaidi na waliokidhi masharti ya kisheria wanahimizwa kushiriki katika uchaguzi huu.

(e) Wito kwa wagombea:

Kwa mujibu wa kanuni ya 17 GN. Na. 571 wakazi wenyе umri wa miaka 21 au zaidi wanaotaka kugombea nafasi za Mwenyekiti wa Kijiji, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa halmashauri ya Kijiji wanahimizwa kuchukua fomu za kugombea katika Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(f) Kuchukua na kurudisha fomu:

Kwa mujibu wa kanuni ya 17 GN. Na. 571 na 574 fomu za kugombea zitatolewa na kutakiwa kurudishwa kuanzia tarehe 01 hadi 07 Novemba 2024 kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

(g) Uteuzi wa wagombea:

Kwa mujibu wa kanuni ya 18 GN Na. 571 na 574 Uteuzi wa wagombea utafanyika tarehe 08 Novemba 2024.

(h) Pingamizi dhidi ya uteuzi:

Kwa mujibu wa kanuni ya 23 GN. Na. 571 na 574 muda wa kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea ni kuanzia tarehe 08 hadi 09 Novemba 2024 na uamuzi wa pingamizi utatolewa kuanzia tarehe 08 hadi 10 Novemba 2024.

(i) Rufaa dhidi ya uamuzi kuhusu pingamizi la uteuzi:

Hii ni kwa mujibu wa kanuni ya 23 (3) GN. Na. 571 na 574 rufaa zitapokelewa kuanzia tarehe 10 na 13 Novemba 2024 na uamuzi wa kamati ya rufaa utatolewa kuanzia tarehe 10 na 13 Novemba 2024.

(j) Kampeni za uchaguzi:

Kwa mujibu wa kanuni ya 27 GN. Na. 571 na 574 Kampeni za uchaguzi zitaanza tarehe 20 hadi tarehe 26 Novemba 2024. Kampeni hizi zitafanyika kuanzia saa 2 kamili asubuhi hadi saa 12 kamili jioni.

Ninatoa wito kwa wananchi wote wenye sifa kushiriki kikamilifu katika mchakato huu wa uchaguzi, kuanzia hatua ya kujiandikisha kwenye orodha ya wapiga kura. Kujiandikisha katika orodha ya wapiga kura ni hatua muhimu inayompa kila mwananchi mwenye sifa haki ya kisheria kushiriki uchaguzi kama mpiga kura au mgombea. Hivyo, Wananchi wanahimizwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ili kutumia haki yao ya kupiga kura au kugombea nafasi za uongozi.

Nafasi zitakazogombewa katika uchaguzi huu ni **Mwenyekiti wa Kijiji, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa halmashauri ya Kijiji** Hivyo, wananchi wenye sifa wanahimizwa kuchukua na kurudisha fomu za kugombea nafasi hizo kwa tarehe zilizoainishwa katika maelekezo haya. Ushiriki wa wananchi wengi katika kugombea nafasi hizi ni muhimu katika kukuza demokrasia na kuhakikisha upatikanaji wa viongozi bora kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mwisho, niwahamasishe Wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi ambayo ni **Jumatano ya tarehe 27 Novemba 2024**, ili kuchagua viongozi bora watakaoongoza.

Imetolewa na:-

DCI. Mariam S. Mwanzalima



MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA

TAREHE 26/09/2024

Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa



Kauli mbiu: Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze kushiriki Uchaguzi.